

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHESHIMIWA  
ENG. EVARIST NDIKILO WAKATI WA UZINDUZI WA  
BARAZA LA WAFANYAKAZI MKOA WA PWANI KATIKA  
UKUMBI WA MIKUTANO WA OFISI YA MKUU WA MKOA  
TAREHE 25/10/2016**

- **Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi - Katibu Tawala wa Mkoa,**
- **Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa - Bibi Catherine Katele,**
- **Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Mkoa,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

***Mshikamano!***

Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa kwa nia njema ya kufanya kikao hiki. Pili nachukua nafasi hii kuwashukuru Mwenyekiti na Baraza lako kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi wa Mkutano huu. Aidha, kwa wale wote waliosafiri kutoka nje ya Wilaya hii ya Kibaha ninawakaribisha na kuwatakia maisha salama mtakapokuwa hapa. Natambua pia uwepo wa wageni waalikwa na kwa heshima ya pekee niwashukuru kwa kukubali mwaliko huu.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Baraza la Wafanyakazi ndilo jukwaa la kisheria la majadiliano ya pamoja kati ya Viongozi na Watumishi katika Utumishi wa Umma kuhusu wajibu na maslahi ya Watumishi. Uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi ni Agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania la mwaka 1970 na ni utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 Kifungu 73(1-3) kinachoelekeza juu ya kutekeleza Sera ya kuwashirikisha Wafanyakazi katika uongozi wa pamoja. Pia Baraza hili hukutana kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Na. 19 ya mwaka 2003 na kisheria Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kinatakiwa kukaa mara mbili mwaka.

Kwa Mkoa huu wa Pwani, Baraza hili lilianzishwa mwaka 2006 na limekuwa likifanyika hadi hivi leo kwa kufuata Mkataba wa Baraza ulioliunda.

### **Ndugu Mwenyekiti,**

Katika kuendeleza mshikamano, hapana budi uongozi uhakikishe kwamba; haki za msingi za Mtumishi kama vile kupandishwa vyeo kwa wakati inavyostahili, kuchukua likizo za mwaka kwa mujibu wa masharti ya ajira, kuwapatia mafunzo ya kuendeleza taaluma zao na haki nyingine za Wafanyakazi bila upendeleo kama nilivyosisitiza wakati wa Sherehe za Mei Mosi mwaka 2016 Wilayani Mkuranga.

### **Ndugu Mwenyekiti,**

Nimekuwa nikizungumzia mara nyingi umuhimu wa Wafanyakazi kuweka bidii katika kujifunza na kujiendeleza kimasomo ili kuongeza ufanisi wa kazi na hivyo kujiwekea misingi imara ya kujenga Utumishi wa Umma ulio bora. ***Mfanyakazi ambaye ni muelewa wa eneo lake la kazi anarahisisha kazi kwa kiongozi wake na yule ambaye sio muelewa wa eneo lake la kazi ni mzigo kwa kiongozi wake,*** hivyo ninawaomba tuzingatie maelezo haya.

## **Ndugu Mwenyekiti,**

Napenda pia kuchukua fursa hii kuisitiza mambo machache ambayo nafikiri ni muhimu.

1. Uwajibikaji ni nguzo kuu ya Mafanikio katika sehemu yoyote ya kazi. Hivyo Wajumbe mnaowakilisha Wafanyakazi wote wa Mkoa hamna budi kuwa mfano katika jambo hili la uwajibikaji.
2. Viongozi wote watoe ushirikiano mkubwa kwa Watumishi wanaowangoza ili kupunguza au kuondoa kabisa malalamiko ya Wafanyakazi mahali pa kazi ili kuleta ufanisi.
3. Viongozi kuhakikisha masuala yote ya maendeleo na matatizo ya Wafanyakazi yanashulikiwa kwa wakati ili kuleta ufanisi, tija na kudumisha nidhamu kazini na hivyo kuongeza ari ya Wafanyakazi.

## **Ndugu Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa na Wajumbe,**

Katika kikao hiki nimeambiwa kutakuwa na Mada zitakazowasilishwa kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2015/2016, na Makadirio ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 na vilevile mada inayohusu Wajibu wa Wajumbe na Umuhimu wa Baraza la Wafanyakazi.

Ni imani yangu kuwa mtasikiliza kwa dhati na kushiriki majadiliano ili mwisho wa siku tupate kuelewa kile kilichokusudiwa. Kumbukeni ndani ya Baraza kila Mjumbe ana haki na fursa sawa na wengine isipokuwa Mwenyekiti wa Baraza. Ni imani yangu kuwa, Ari, Fursa na Heshima vitatumika kwa

busara na hekima kubwa ili mwisho wa siku tuweze kufanikisha malengo tutakayojiwekea.

**Mwisho,**

Matarajio yangu ni kwamba, kila Mjumbe aliyeko hapa atatimiza wajibu wake ili kuweza kufanikisha azma ya Serikali ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Naamini sote tukifanya kazi zetu kwa umakini tutaweza kutoa mchango wetu kikamilifu katika kufikia malengo ya Serikali ya awamu ya tano ya ujenzi wa viwanda na uchumi. Katika kukamilisha azma hiyo, Watumishi wa Umma wanaowajibu mkubwa wa kuongeza kujituma na kuwa waadilifu.

Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka kwamba Baraza la Wafanyakazi Mkoa wa Pwani limezinduliwa rasmi.

**“MSHIKAMANO DAIMA”**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**